

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

(CKRC)

Verbatim Report of

DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL,

**EMUHAYA CONSTITUENCY, HELD AT MUMBOHA CHURCH OF GOD ON
14TH OCTOBER 2002**

ON

14TH OCTOBER 2002

FINAL COPY

**DISSEMINATION OF REPORT AND DRAFT BILL, EMUHAYA CONSTITUENCY, HELD AT MUMBOHA
CHURCH OF GOD, LUANDA ON 14TH OCTOBER 2002**

Present

1. Kavetsa Adagala - Commissioner

Secretaria Staff in Attendance

1. Vincent Watako - Assistant Programme Officer
2. Patricia Mwangi - Verbatim Recorder
3. Agnes Ayuma - District Coordinator

CCC's Members

1. Arthur Etele - Member
2. Arthur Imbira - Member
3. Christorper Kwache - Member
4. Getrude Obulutsa - Chairperson
5. Bettina Okumbe - Member
6. Dorah Ingolo - Member
7. George Oredo - Member
8. Cllr. Gilbert S. Opanga - Member
9. Rev. Bishop Byrum Makokha - ACK Maseno North
10. Hon. Sheldon Muchilwa - M.P. Emuhaya

The meeting started at 9.45 a.m.

Agnes Ayuma: Wale ambao mme-register ningependa muje karibu wale watakaokuja baadaye ndio watakaa nyuma ndio tuweze kuanza haraka haraka. Florence, akina mama wachukue mstari wa mbele.

Habari zenu yes, (vernacular) we shall start off immediately. Kuna mzee anaweza kutuomba. Mzee utatuomba?.....(Inaudible)

Agnes Ayuma : Thank you Mzee, nilisikia maombi yote Mzee alituomba ambayo alisema tutatengeneza maneno ambaye itatusaidia badaye sivyo? Karibu bwana Commissioner.

Com. Adagala:(Vernacular) so tuta-prevent lakini tutakata kata kwa sababu hii mambo inafaa wale watu wanaamini na wana-interest, kama interest ni ndogo ni vigumu kuendelea na kuna vitu vingine vinafaa kuelezwa kama watu wako wengi, sasa hiyo tuta-skip kwa sababu it doesn't make sense to do it just to a few people.

Mimi ni Commissioner Kavetsa Adagala na alikuwa huku kwa civic education? Nani alikuwa huku for hearings? Which Commissioner was there? Asante, akina nani walikuwa hapa kutoa maoni? Pengine watu wa Emuhaya wanajua mengi, huyu ni Vincent atajitambulisha.

Vincent Watakao: ... (Vernacular) Jina langu ni Vincent Watakao.

Com. Adagala: Huyu mama.

Patricia Mwangi: Habari zenu?

Audience: Mzuri.

Patricia Mwangi: Mimi naitwa Patricia Mwangi.

Com. Adagala: Okay, haya mkiangalia kwa Katiba yenu hapo mwanzo, table of contents. Okay, hapo table of contents, tuangalie katiba ina sura ishirini. Tuzungumze kwa lugha gani? Kiswahili kwa sababu tukichukua tafsiri itakua shida. Kuna mtu ambaye haelewi Kiswahili? Haya, hapa kuna kiti kinaitwa preamble, table of contents don't go ahead hapo tu kwa orodha. Kuna preamble, hiyo inachukua maoni na maono na vile Wakenya wangependa Kenya isimame, nitaizungumzia hapo. Haya ile inafuata ni ukubwa au ukuu wa watu na Katiba, vitu viwili pekee viko na maana kwa Kenya.; wananchi na Katiba. Hakuna kitu kingine kikubwa kuliko hii, wananchi na Katiba.

Halafu hiyo sura ya tatu inaeleza Jamhuri ya Kenya ni nini, iko wapi, ina upana gani? Hayo yote iko hapo na nani wako hapo ndani na vitu kama hivyo. Capital: tutazungumzia hiyo. Halafu sura hiyo ingine inafuata, hiyo ndio inazungumzia lengo na nia ya Kenya. Kwa Katiba ya leo hivi vitu vyote havipo, hii sura ya tatu yote haiko isipokuwa inaanza tu Kenya is a sovereign

republic halafu hivi vitu vingine haviko. Sasa hiyo ina nia na lengo.

Halafu uraia wa Kenya inafuata kukiwa na nchi lazima iwe na raia na raia wa Kenya ni nani, hasa Mkenya ni nani? Halafu kuna sehemu hapo ambayo kwa Kiswahili wanaita Ukatiba kwa tafsiri ile ya Kiswahili inaitwa Ukatiba na hiyo ni sawa hata kuliko hii bill of rights, hiyo ukatiba kwa sababu hii inazungumzia vile wananchi wanaishi na Katiba, nini mtu anapata kwa Katiba na yeye anapeana nini kwa Katiba. Hapo ni sehemu ndefu lakini tutapitia.

Halafu kuna ile uwakilishi wa watu kwa sababu nguvu ni za watu, kuna uwakilishi wa watu kwa sura ya sita, uwakilishi wa watu, nguvu ni ya wananchi halafu wanatoa kwa wengine kuwakilisha, sio wale ambao wanaakilisha wana nguvu kuliko wananchi, pengine hata itafaa tubadilishe hii kitu Mweshimiwa iwe mtumishi kwa sababu uongozi utaenda kubadilika. Hiyo sehemu yote ni kuhusu mambo hayo.

Halafu tunaingia kinaganaga kwa ile uwakilishi tatu wa serikali kuna mapacha matatu hapa. Legislature, kuna Executive, kuna Bunge, kuna Urais halafu kuna Mahakama, tatu. Haya mapacha matatu inafaa ilingane. Kwa Katiba ya sasa, kuna Katiba ya uhuru ile ya 1963 ile ilitupatia uhuru, sio hii uhuru ingine inatembea sasa ni ile ya 1963. Kwa hiyo ilikuwa imetengenezwa sawa lakini waliweka bolts na spanner na wakafanya spanner job na panel beating halafu ikawa Rais alienda juu sana, sehemu ya Rais na inafaa ziwe zilingane hapo. Sasa hiyo tutazungumzia. Executive, nimezungumzia hiyo. Chapter ingine ni ya Executive, ingine ni ya Mahakama.

Okay, kuna kitu kinaitwa devolution of powers yaani kuzambaza nguvu. Zilikuwa zimewekwa zote pamoja. Tutazungumzia hiyo zaidi lakini sasa inakaa izambazwe ili iwe kila mahali na isiwe mahali pamoja. Kama Nairobi inaguvu zote na pia hiyo kiti cha Rais ina nguvu zote wakati huu, sasa inafaa izambazwe ili hiyo nguvu irudi kule ilikuwa. From 1963 wananchi walikuwa na nguvu lakini ilitolewa baadaye na amendments.

Halafu ardhi na mali inafuata, mnaiona? Ardhi na mali inafuata na vile tutakaa, vile tutajipanga kwa ardhi na mali. Halafu kuna mazingara na mali asili ya nchi na vile italindwa na vile watatumia na vile tutaitumia kustawi.

Halafu pesa ya uma, halafu utumishi wa uma pia iko hapo. Halafu ulinzi. Chapter 14 ulinzi na vile Kenya itakaa kwa usalama.

Halafu kuna njia ingine pia ya kukaa kikatiba na hiyo ni Tume, tumetunga Tume kumi na zimekaa hapo tutazungumzia, halafu kurekebisha Katiba na vile itatendeka. 19, ni kufafanua tu vile tunaweza kuangalia hiyo na kuona vile tutafafanua hii Katiba.

Halafu sura ya ishirini inazungumzia vile tutavuka kutoka Katiba ya sasa kuenda kwa hii ikipitishwa, kuenda kwa mpya, ni kama daraja vile itapita kutoka kwa moja kuenda kwa ingine na tutazungumzia hiyo. Halafu kuna vitu vinaitwa schedules, ni kueleza kinaganaga mambo iko hapa na tatamweleza tukiendelea tuone vile itakaa. Haya vile tumeanza, tumewacha sehemu fulani ambayo nitaeleza baadaye watu wakiwa wengi, hiyo ya process, otherwise tutaendelea tu na Katiba mpaka tutachukua break halafu tutaeleza hiyo process na tuendeleo pia na Katiba. Kuna swali lolote au comment yoyote? Tutaendelea hivyo, tutakuwa

tukisimama simama ili mkiwa na comment mlete mbele au proposal, hasa ni proposals tunazungumzia. Hizo sura ishirini zimeelewaka? Zimeeleweka? Nataka tuzielewe ili tuende moja moja na tujue tutakuwa tukipita hatua kwa hatua, sio kuvuka mbele au kurudi nyuma au kuendelea, au kufanya nini lakini moja kwa moja tutakuwa tukiendelea. Okay, any comment, where is the District Coordinator, Agness. Where is the Chairman of the 3C's? Chair ako wapi? Are you the chair, chairman ni nani?

Chairman, I am very disappointed that you are late and that the room was empty when we arrived. There is no explanation for it, the room was empty?

Kuna mtu ambaye anataka kusema lolote? Haya tuendele... (Inaudible)

Oko Lukose: Chairman hatujui kama mpango itakuwa namna gani kwa sababu nilikuwa huko Church of God, Kima na nikapeana memorandum huko ambayo nilifanya update baadaye na baada ya draft kutoka nimefanya some comments, kwa hivyo sijui kama mpango ya hapa itakuwa vile tumeandika majina huko nje tukiingia, tutakuwa na nafasi ya kuzungumza juu ya hii ama itakuwa tu hapa kwamba yule anayesimama amasema vile navyoona kwa sababu kuna comments nataka kutoa kutoka mwanzo mpaka mwisho ya hiyo draft.

Com. Adagala: Jina lako?

Patricia Mwangi: Say your name?

Ako Lukose: Jina langu ni Ako Lukose.

Com. Adagala: Lukose asante wewe umefanya homework yako kwa sababu hizi zilikuwa kwa magazeti, bill ilikuwa kwa magazeti na wale walinunua natarajia wamesoma, kama una-comments ni mzuri lakini hizi sio hearings, vile ilikuwa hearing. Hii ni kukagua na vile umekagua utakuwa ukitoa comments zako kwa kila sehemu tunazungumzia, okay? Tutaenda chapter by chapter na utatoa maoni. Kila mtu atatoa maoni, mjisikie wazi, mjisikie kama mnaweza kuendelea na kuzungumza bado kutoka kwa majadiliano na hii ni kukagua sasa vile kama imekaa hivi au ni vizuri au la. Okay, imeeleweka Mr. Lukose?

Mr. Lukose: Imeeleweka.

Com. Adagala: Okay. Comment ingine? Tumelewa vile tutaendelea, nikikosa kupata jibu nitawacha.

Oketch Elffas: Kwa hivyo comment ambayo imefanywa, tusema chapter five.

Com. Adagala: Your name.

Oketch Elfas: Oketch Elfas. Tukifika kwa chapter five for example, yoyote ambaye atakuwa na comment chapter five atasimama aseme? Asante.

Com. Adagala: Ndio tutafanya. Okay, tukifika chapter fulani ukiwa na comment utasema lakini msiruke ruke mbele kwa sababu hatuwezi kuendelea vizuri tukiwa hivyo. Macho yangu hayaoni vizuri sasa huyu kijana atakuwa ananisaidia, yeye ni wakili pia, yeye ni Programme Officer, tutakuwa tukifanya presentation together lakini vile macho yangu hayaoni sasa mtanihurumia hapo au mnisamehe lakini tutaendelea, yote iko hapa lakini kwa kinaganaga atakuwa ananisaidia kwa kusoma utaratibu.

Kuna kitu kinaitwa preamble, present Kenyan Constitution doesn't have a preamble basically Mzungu hakuona maana ya kuweka preamble because preamble inaweka mambo ambayo watu wanafikiria. Maono ya watu, lengo lao na mipango yao ya kuishi na vile tulipata hii Katiba kutoka kwa mwingereza hakuona maana ya kuweka hiyo sasa Katiba ya sasa inaanza tu, Kenya is a sovereign republic lakini hapa Katiba ya mambolea ni ile ambayo ina preamble. Tangu ile ilikuwa Katiba ya kwanza kuandikwa in full ya United States walipokuwa wanapigana na Wingereza hiyo inaeleweka, modern republic, jamhuri za kisasa zina preamble na hiyo preamble jamhuri inapata nguvu kutoka kwa watu. Sasa vile tunaendelea pengine niwambie ile Katiba ya 1963, Britain walitengeneza tu modal Constitution, sasa kama Ghana ilitaka uhuru wanatoa hiyo kwa shelf wanaweka hiyo mambo inalinganishwa na Ghana, Tanganyika inafika wakati pia wanatoa hiyo wanaweka. Yao ilikuwa kupeana republic, watu wachukue nchi nzao, sasa hawakuwa na haja na kitu kingine chochote. Sasa ndani ya hii republic walitengeneza ilikua haina watu ndani, ni kama haikuwa na watu ndani na hapa ndio unaona tumeanza, we the people of Kenya. Wengine tulifikiria iwe we the people or we the peoples of Kenya tulikuwa na majibiano. Sehemu ndogo hiyo ilikuwa wiki nyingi sana kutengeneza na ndio muhimu kwa sababu Katiba yote iko kwa hii sehemu, kitabu changu ni ukurasa wa kwanza. Katiba yote iko hapa ndani, hii ingine sasa ni kufafanua na kuendelea.

Preamble ni kitu muhimu na wengi mlituambia we want a preamble in our Constitution, si hivyo? Ndio mlisema hiyo kwa sababu mlikuwa mmepata civic education mnajua, mnaona vile inaendelea, Katiba zingine sasa mkasema tunataka tuwe na preamble. So for the first time in Kenya we are constituting our nation with the people, the people are constituting the nation. Hapo mbeleni ndio uliona saa zingine vitu vinatendeka hata bila kuulinza wananchi kwa sababu wananchi hawako kwa Katiba, lakini siku hizi lazima au kwa hii Katiba lazima wauliza wananchi na hata nchi imebadilika kidogo kidogo watu pia wameanza kufikiria hivyo, lazima tuulizwe. Lakini miaka hii yote walikuwa wanauliza kwa nini hatuulizwi? Kwa nini watu wanaendelea tu au viongozi wanaendelea tu bila kuuliza sisi. Vitu vikubwa na vitu vidogo, kama hivyo vitu vikubwa vya IMF loans na vitu kama hivo, Minister alikuwa tu anaenda ana-sign halafu sisi tunalipa taxes, kodi ambayo inaenda kulipa hiyo deni na hatukuwa tunaulizwa. Sasa hapo ndio inaanza, we the people of Kenya, sisi wananchi wa Kenya. Hapo mwanzo inazungumzia kuhusu vile tuko watu tofauti tofauti, diversity tofauti, wanawake kwa wanaume, vijana, kabila tofauti tofauti, walemavu, watu aina

tofauti, yote hayo tofauti, kabila kubwa, kabila ndogo na zote zipo. Hapo ni diversity, hiyo inasema... tunakubali tuko watu tofauti tofauti, hiyo ni kitu muhimu sana, si tunasema tutawacha hii lakini hiyo inasema kila mtu awe mtu wa aina gani akiwa Mkenya yeye ako hapa, we recognize that.

Kitu kikubwa tuliambiwa na watu, tusiende tukagawe Kenya, tusiende tukaweke mambo ambayo itagawa Kenya. Sasa hapa inasema sisi ni nchi moja ambayo haiwezi kutawanyika, tutakaa nchi moja, tutakaa hivyo bila kutawanyika. Hapo tukaambiwa na watu, walitaka watu walindwe mtu binafsi, familia na pia jamii iwepo ifadhiwe kwa Katiba. Halafu tukaambiwa kuna maneno Fulani ambayo ni muhimu sana, tuna hiyo uhuru, demokrasia, sheria kutawala na pia hiyo ya human rights kama social justice, hiyo ya haki ya binadamu na pia tuna haki, kuna ile haki ya utovu. (vernacular). Hiyo ni kama mtu hawezi kukunyanganya, nikija nikitoa tovu yako utakufa kwa sababu ni kama mwili yote imejengwa na imewekwa hapo eeh, hii ndio kifuniko. Wazungu wanaita belly burtons, hiyo ni kama the burtons that tie up the whole body, lakini hiyo ni kitu hatuwezi kutolewa. Kuna haki ya kuunda serikali yetu na pia sasa tunatengeneza na kutekeleza Katiba hii na kujipeana wenyewe, tunajipa hii Katiba na pia tunapeana kwa vizazi vijavyo. Hii ni yetu wenyewe, ni kama unazawadi unajipea wewe mwenyewe na pia inapea watoto wako. Kidogo ni urithi, tutawacha watoto wetu watarithi na tuliambiwa na watu hakuna Mungu kwa hii Katiba yetu ya sasa ndio tunayumba yumba, tunaenda huku, tunaenda kule hakuna msimamo na wakasema tuweke Mungu kwa Katiba. Wengine kama mimi nilitaka vile tulikuwa tunajadiliana, nilitaka ianza na hiyo; Oh God of all creation halafu tutaenda...we the people of Kenya believing in the God of all creation halafu tuendelee, hiyo ya nyimbo ya taifa lakini mwingine akasema tuweke hapa kati kati kama supremacy of God, tutafanya revision hiyo tena mpaka tukaja hapa ndio tukafanya God Bless Kenya, Mungu ibariki Kenya. Kwa ile ya Kiswahili inasema Mungu ibariki Kenya. Katiba ya sasa iko hivyo kwa sababu tunajua Mungu mwenyewe mwishowe ndio yeye ana mwanzo na mwisho, yeye anaamua na yeye ndio anatupea hata maisha hii tunayo, hata hii nchi tunayo ndio alitupea. Kama ya South Africa inasema “go sisi kele South Africa” pia wao wanaweka hata ya Amerika iko na hiyo, God ndani ya Katiba yao. Kuna swali lolote hapo kwa preamble, jisikia, kuja, nataka tufanye hivi, ukitaka kuzungumza njoo tu usimame hapa, mara moja usingonjee.

Mr. Lukose: Mwenyekiti mimi nasema kuhusu preamble.

Com. Adagala: Taja jina lako.

Mr. Lukose: Jina langu ni Lukose, iko kwa register pale. Kuhusu preamble mimi nafikiri ni kitu ya maana sana kwa kila Katiba ama kitabu au kitu kingine sawa pretence kwa sababu preamble itaonyesha, sisi ni nchi kutokana kwa sababu gani na sisi ni wananchi wa Kenya tuna uhusiano gani kama watu mbali mbali, wa kabila hii, kabila ile. Ni kitu gani ambacho kinatuweka kuwa pamoja kama watu wa nchi moja. Kwa hivyo preamble, mimi sidhani kama niko na mambo mengi ya kusema nafikiri inafaa hii preamble kuwa kwa Katiba kwa sababu ndio itaonyesha ni mambo gani ambayo yanafuata katika hiyo Katiba.

Com. Adagala: Asante mzee, vile ningetaka tuendelee si comments, kila kitatusaidia sana ni kama una proposal. Mzee amefanya vizuri, kama unaunga mkono ni sawa lakini leta proposal, leta pendekezo juu yake. Kuna vitu vingi sana vinakuja, very detailed so ni vizuri umesema hivyo lakini kama kuna mtu ambaye angependa jambo hapo liongezwe kwa preamble njoo mbele na sitaki usimame kama mwingine, simama mwanzo ili uje mbele. Kuna mtu mwingine anataka ku-comment kuhusu preamble, kuleta maoni mengine kwa preamble? Kunayo? Njoo mbele, nataka tupate utaratibu wa laini hapa.

Isaac Malanya: Naomba ...

Com. Adagala: Ninataka utajie kuhusu mambo ya preamble pekee.

Isaac Malanya: Hapana implementing the Constitution.

Com. Adagala: No, we are talking about the preamble. Nimeeleza sitaka turukeruke, hiyo itakuwa na nafasi yake, keti tu utapata nafasi. Kuna mtu mwingine? You know hakuna mtu wa kukubembeleza mzee. Habari yako mzee?

Rev. Enos Ochola: Rev. Enos Ochola. Mimi vile ninavyoona, ntoa pendekezo kwamba vile maandishi ya preamble yalivyo iwe hivyo hivyo maana kwa miaka thelathini na tisa tumekuwa katika enzi ambayo wengi sisi hatukueleza ni kitu gani kinachotendeka. Basi, vile ninavyoona wenzangu wakikubaliana na mimi tulitaka hilo neno, tulitaka preamble na imekuwepo na vile ilivyo ni fupi na ni mzuri. Asante.

Com. Adagala: Haya maoni yako ni tofauti, tofauti ukiwa na nafasi nisiangalie preamble ya Constitution of India ni fupi hata kuliko yetu, ni kitu kama six short sentences na ina mambo yote hapo. Ni kama nisema vile tuko na, watoto hawa ni watoto wa nani? Msiwafukuze ni watoto wa nani. Wa Wanyore, sawa, wakiweza kuketi na kukimya itakuwa vizuri.....(vernacular) lakini itakuwa sasa wote watataka. Haya, preamble ya India iko fupi hivyo, Kenya tumekaa vibaya sana kwa sababu hata hatukujua Katiba yetu inasema nini, ni kama kusema wewe ni Mkristo na hujui jambo hata moja la Bibilia au Muislamu na Koran haujui. Hii ni kitu cha kuamini, Katiba si makaratasi tu, vile iko tu sasa ni makaratasi.

Haya tuendelee? You are not going to stand one by one, tutatengeneza laini hapa, hivyo ndio tutaendelea ndio iende haraka. I don't want any after thought, sitaki after thought nataka watu wa-pay attention na waje mbele.

Reuben Anjeo: Reuben Anjeo.

Com. Adagala: Okay, proposal.

Reuben Anjeo: Niko na-propose kwamba already tuko na wimbo wa taifa. Wimbo huu ndio unafundishwa watoto kutoka

wakika wadogo mpaka wamekuwa wakubwa ambao inafanya kwamba tunashikilia haya, tunayakumbuka kila siku.

Com. Adagala: Pendekezo.

Reuben Anjeo: Preamble, sioni kwa nini tungetengeneza preamble ingine ikiwa kwamba tuko na huo wimbo ambao bado inatuunganisha sisi kama watu wa Kenya. Sasa tutakuwa tuko na wimbo kama preamble na huu tena mambo mengine hayo tofauti.

Com. Adagala: Ulikuwa hapa wakati wa kutoa maoni? You were here when hearings were going on and you said that?

Reuben Anjeo: I was not.

Com. Adagala: Because we are not in after thought now.

Reuben Anjeo: I thought that were going back and correct what I said.

Com. Adagala: What did you say then?

Reuben Anjeo: I didn't talk about preamble.

Com. Adagala: It is okay. Imeandikwa chini instead of... okay, tuendele. Tutaenda chapter by chapter usiende mbele kwa sababu tuko watu wengi, this is mass education so if you go ahead it will be very difficult na nimesikitika kwa sababu naona wanaume wengi sana hapa.... (vernacular). The District Coordinator should not have put it on a market day. Agnes?
And the Chairman you should not have put this day on a market day.

Sura ya pili.

Getrude Obulutsa (Chairman: ...)(Inaudible)

Com. Adagala: Chairman control yourself. Why did you put this on a market day?

Getrude Obulutsa: The date was given by the Commission and we could not change it.

Com. Adagala: Change it? You could have told them it is a market day, we could have easily done Vihiga and then the day for Vihiga would have been this time. Haya wanasema wanawake wako market. Wanawake ndio wanaenda market? We should say that they are the bread winners of Bunyore, okay, sasa bread winners watajuaje Katiba na wao ndio bread winners?

Haya, sura ya pili unajua tunamchukua vile nyinyi wenyewe mnajichukua, sasa kwa vile iko hivi itakuwa low intensive vile mtaichukua, vile nimeanza on a low note, so ikienda hivyo itakuwa low note. Haya kuna vitu viwili nimeeleza ambavyo vipo muhimu; Katiba na wananchi, kuna vitu viwili muhimu, wananchi na Katiba. Hakuna kitu kingine kikubwa kuliko hicho kwa Kenya. Hakuna mtu mwingine mkubwa kuliko wananchi, hakuna kitu kingine kikubwa kuliko Katiba. Wananchi wana tengeneza Katiba waliunda Katiba na Katiba inalinda wananchi. Nataka muelewe hii sana kwa sababu imekuwa kama kuna watu wengine ambao walikuwa above the Constitution, above the law. Hakuna kitu kama hicho kwa hii Katiba ni wananchi ndio wananguvu na hivyo ndio inasema hapa. Nguvu zote za Kenya ni za wananchi zile ziko kwa Katiba na wananchi wanatekeleza hizi nguvu kwa kupeana kwa wale ambao wanawakilisha na hiyo ni Bunge, Rais na Mahakama. Mmeona tukiwa na shida na mahakama kwa sababu wanafikiri wao wako above na hawako kwa sababu wanapata nguvu kutoka kwa nyinyi hata kwa Katiba iliandikwa vibaya au ilirekebisha ikahariba nguvu zao zinatoka kwa nyinyi. Sasa wanasema wananchi wa Kenya wasizingumzie sehemu ya mahakama. Sasa ni kama wamepiga marufuku watu milioni thelathini kutozungumzia mahakama. Sasa kidogo ni kama Kenya ni jela sasa, mnajua hivyo? Kwa sababu watu wa mahakama, Majajis wametoa hukumu yao na wamesema msizungumzie, sasa hiyo ni guard, wameshona midomo, mnakubali? Na nguvu ni zenu. Hii ni kitu wao watafaa wajifunze kabisa nguvu ni za wananchi. Sasa hiyo maelezo iko hapo kwa hizo paragraph ni ya kueleza kinaganaga.

Kenya sasa tuseme tunaunda Kenya kwa sababu haikuwa imeundwa kamili, sasa Kenya mzingi wake ni ukuu wa Katiba si ukuu wa kitu kingine au ukuu wa hii na ile na ile ya Mungu tumeshasema, God bless Kenya. Sasa sa zingine watu wanasema lakini Mungu yuko, tume-recognize Mungu. Mungu ibariki Kenya lakini vitu vyote viko chini ya Katiba hakuna mtu ako juu ya Katiba, hakuna jambo ambalo liko juu ya Katiba, hakuna tendo ambalo litakuwa juu ya Katiba. Mkisikia Military Government mjue hiyo inakuwa sasa wamevunja Katiba. Kwanza Military Government ikifika kiti kimoja wanatupa kwa moto ni Katiba, Amin alipochukua Government kwa Obote, kiti kimoja alikanyaga ni Katiba. Katiba ikitoweka sasa ni serikali ya imla au ya majeshi, mnaelewa? Haya.

Constitution inashikanisha watu wote, nguvu zote, wakuu wote, inashikanisha pamoja. Hiyo ya kuteleza Katiba haitakuwa kitu cha kupinga, Katiba inatekeleza kwa njia fulani na iko hapa vile itatekelezwa na hakuna mtu atakuja kusema hiyo haiwezekani. Hiyo ndio ukuu wa Katiba.

Kuna masheria zingine saa zingine sheria ya jamii fulani au mtu mwengine anaunda sheria kwa nyumba yake anasema sheria ya nyumba hii ni fulani lakini ikigongana na Katiba basi itatupiliwa mbali, Katiba ndio sheria kuu. Itafafanuliwa na kutekelezwa na kusimamia au kudhamaniwa utawala mzuri, wema, haki za binadamu na uongozo wa sheria na itatengenezwa ili isiwe na vitu

fulani ambavyo litaifanya kuwa ngumu kueleweka kwa wananchi. Hii Katiba ingine tunayo ina lugha ngumu sana hata mwishowe wakili wenyewe wakisoma wanaielewa halafu wanafika mahali fulani inakuwa shida hata Professor Ghai anasema...

Na pia kwa ile lugha ya zamani na ni ngumu sana. Lakini hii yenye tumeandika ile mnaona mkisoma, mnaweza kusoma, si hivyo? Ukiwa hata mtu wa Standard Eight unaweza kusoma na dictionary pengine kidogo hapa na pale lakini mtu wa High School anaweza kusoma halafu tutatoa ya Kiswahili na tunafikiri itakuwa Kiswahili raisi na pia itakuwa raisi kusoma. Nataka watu waelewe, hakuna maana kuishi na sheria ambayo hauwezi hata kuelewa, si hivyo?

Hiyo sasa watu wanafaa waone hii Katiba inaendeleza na watu wa mahakama. Judges are the ones who should make sure that this Constitution itakuwa enforced na mahakama wao wamesema wanapinga Katiba sasa mnaona vile tuko? Wamesema tusiendeleee na tunaendelea kwa sababu ni nonsense, ni upuuzi vile wanasema. Ile ya kuleta serikali ambayo si ya Kikatiba ni haramu, hatia na haikubaliwi, na serikali ambayo si ya Kikatiba ni imla au ya Majeshi au ile ya kutokuwa na sheria. Tukizungumzia kuhusu sheria ya Kenya kwa jumla, ya kwanza ni Katiba. Sasa hizo sheria za Bunge zinadhipitishwa na Bunge, mswada inakuweko halafu inapitishwa inakuwa sheria hizo pia, mila ya Kiafrika na sheria za Kiafrika, ya Kiislamu na ya Kiindi. Halafu kuna ingine inaitwa common law halafu ile ya East Africa vile mnajua tuko kwa East African na kuna East Africa Parliament. Nafikiri wengi mnajua Shama Lab ako huko na hiyo ya kimataifa ambayo imekubaliwa kimataifa, hiyo ya treaty na vitu kama hivyo na conventions.

Parliament itachukua miaka miwili kutengeneza na kulinganisha hii sheria yote ili iwe kitu kimoja isiwe na kugongana gongana na hayo mambo yote iko kwa kitu tunaita schedule six. Mkiangalia nyuma baadaye sio sasa, ni kitu cha kuketi na kusoma, wameeleza kinaganaga kile Parliament itafanya, kile Bunge itafanya kwa miaka hayo miwili. Hii Bunge ijayo kazi yao kuthibitisha hii Katiba, kazi yao itakuwa kutekeleza sheria na kujadiliana sheria ambayo na vile Katiba itatekelezwa, miaka miwili, mnaelewa? Watakuwa na miaka miwili, hiyo ni part of transition provision. Two years Parliament will discuss this. Are there any questions there? Si questions, additional proposals au haieleweki?

Speaker: Inaeleweka.

Com. Adagala: Hatuko hapa kuelewa tu, tuko hapa kukagua na kuona kama kuna mashimo, kama kuna kitu kimewachwa nje au kitu ambacho si kizuri, au kitu ambacho kinaweza kuwa kizuri zaidi au bora zaidi. Nataka muwe alert, kuna vitu hapa ambavyo in this chapter which we have just done which you have to be very alert on.

Kuja mbele, panga laini hapa ...

Jairus Lusuli: Jina langu ni Jairus Lusuli. Ningependa nipitie kwamba katika wakati Bunge waliketi wakapeana mswada kwamba Katiba itengenezwa upya, ni sehemu gani ambayo Bunge ilipitisha au ikasema iwachwe, isiwe discussed ndio sababu

Madam Commissioner amesema kwamba Mahakama au Judges hawataki wananchi wa-discuss mambo kuhusu judiciary na wakati Bunge ilipopitisha mswada kwamba Wakenya wapeana maoni halafu watengeneze Katiba mpya, kuna sehemu yoyote ambayo haikutaka ijadiliwe hapa Kenya.

Com. Adagala: Vile mzee amesema ni vizuri na pia nataka kusema kitu cha kushangaza hapa kwa Katiba wao ndio wamepewe ile ya kulinda Katiba. Sijui Lumwai...(vernacular) mnajua hiyo hadithi.(Vernacular) anafaa alinde ni kama vile wanasema kuweka fisi alinde kondoo au alinde kuku haiwezekani. Wao ndio gatekeepers na wao ndio wamepinga. Kitu kikubwa ni kitu kinaitwa self interest na hii society tumekuwa nayo imekuwa ya self interest ya watu wakubwa na hiyo ilionyesha wazi.

Rev. Dennis Ochola: I am Reverend Dennis Ochola, kikundi cha Forum for Understanding. Chapter hii inashuhudia kwamba tulizungumza hatukuwa tu, tulizungumza tukajadiliana na kila kitu ambacho tuliweka ndani, tuliona inafaa kwa maana yale ambao tunatengeneza wakati huu si yetu tu, ni ya vizazi ambavyo vinakuja. Tukiharibu leo basi kesho ni lawama kwetu.

Com. Adagala: Ngoja kidogo. Nikiangalia hapa nyuma, una Constitution yako?

Rev. Denis Ochola: Yako iko wapi?

Com. Adagala: Ukiangalia hapo inasema the law of Kenya, na kuuliza hii kwa sababu ya swala yako. Inasema Constitution, parliamentary laws, African Customary Law, Islamic and Hindu law na hizo zingine kadhalika. Kuna kitu ambacho hakiko hapo?

Rev. Dennis Ochola: Hata zilikuwepo ndani kabla Wazungu hawaja....

Com. Adagala: Okay, nakuuliza kwa sababu ya hii. Kuna kitu ambacho hakiko hapa?

Rev. Dennis Ochola: Hakuna kitu ambacho hakiko hapa kwa maana sheria, mtu ndio anageuka. Mungu ndiye alipeana sheria na ...

Com. Adagala: Anasema hapa hapa tu na kweli kuna Biblia na ina sheria. Iko hapa?

Rev. Dennis Ochola: Ipo.

Com. Adagala: Okay sit down tutazungumza zaidi. Usizungumza ukiketi, mzee keti hiyo jambo ambalo hata tutakucha....

Rev. Dennis Ochola: I am not following what you are saying.

Com. Adagala: I am talking to you very clearly. We have something called Christian law and then we have something called living in time of praise halafu mnasema hiyo mambo ya law. Unajua Wakristo wako na hii, the law of Moses and then there is a time of praise, Christ coming. Waislamu wameifadhi yao hapa, ya Wakristo iko wapi?

Rev. Dennis Ochola: Ina watu wenyewe.

Com. Adagala: Ina watu wenyewe. This is the law of Kenya, okay, wacha huyu dot.com azungumze kidogo nione atasema nini.

Joel Akaki: My name is Joel Akaki, I am a teacher by profession. I am looking at section 5 (ii), it says the Parliament shall within two years make some amendments on the Constitution in reference to those laws you have said there. So I am wondering, will they be doing it with consultation of the people or they shall be doing it...

Com. Adagala: Mwenzangu Mwalimu, it is a time for you to propose. The Constitution gives you more power than wondering.

Joel Akaki: I am proposing that they should consult us before they can make any other changes or enforce any other of these laws here.

Com. Adagala: How do you want us to conduct it?

Joel Akaki: Through a forum or something of that kind.

Com. Adagala: You only want to be informed, remember these people have your power, you are the one with the power. You only want to be informed? They are your servants.

Joel Akaki: No.

Com. Adagala: But perhaps that is what you want.

Joel Akaki: They should ask us and we should give our views as far as the amendments they will be making.

Com. Adagala: There is no making in the Constitution....

Joel Akaki: Okay let me use the common language. They should consult us.

Com. Adagala: You really have to say it...(Inaudible)

Joel Akaki: Through the Commission.

Com. Adagala: Umekuwa hapa kwa hearing?

Joel Akaki: Yes there is this Constitution Commission, they should organise so that we can have such a forum as this one where we can be consulted on these amendments.

Com. Adagala: You see you are saying less than you want. You want to be informed, then you want to be consulted, then after you are consulted.

Joel Akaki: ...(Inaudible)

Com. Adagala: It is not they, it is you. I want you to speak, this is part of what you have to realize life has changed. I want you to say, you were here for Civil Education how are the people consulted.

Joel Akaki: Through discussion like this one.

Com. Adagala: And then?

Joel Akaki: May be their views are taken on board.

Com. Adagala: And then.

Joel Akaki:(Inaudible)

Com. Adagala: No, they vote and how do they vote?

Joel Akaki: Through a referendum.

Com. Adagala: Through a referendum. That is what I wanted you to say, now you are forcing me to do civic education again.

You have to say it yourself, propose.

Joel Akaki: So they should come to us and they should hear our views after that we should vote through a referendum like this one.

Florence Asila: Thank you. My name is Florence Asila. Section 5 talking of the laws of Kenya nilikuwa nataka hii iwekwe in such a way that when these other laws are in conflict with the Constitution, the Constitution prevails, isn't it? Lakini vile imewekwa hapa nilikuwa naona they are all laws of Kenya and applicable and I was seeing a bit of confusion sometimes when say, African Customary Law is strong and is at variance a bit or I need reprieve from being suppressed with African Customary Law can I get reprieve in the Constitution. Nataka iwekewe hivyo, sioni kama ilikuwa imetoka hivyo.

Com. Adagala: ...(Inaudible)

Kaiser Amatalo: I am Kaiser Amatalo. I wanted to say that for example we have said the laws of Kenya comprise the Constitution and then may be you say acts of Parliament enacted under the Constitution. Tukifika sehemu ya c na d, tunasema tu African Customary Law halafu tunasema Islamic and Hindu.

Com. Adagala: You have to go through all these....and the second one you asked me Act of Parliament...

Kaiser Amatalo: Tumesema vizuri acts of Parliament enacted under the Constitution lakini tukisema C na D tunasema tu African Customary Law halafu tunasema Islamic and Hindu personal law but there is this argument, labda hizi African customary Law, Islamic and Hindu personal law zinajaribu kufinya Constitution, tutazikubali? Lazima ziwe zinakubaliana na Constitution.

Com. Adagala: Hapo tumesema ile inagongana na Constitution, Constitution is supreme lakini kuna Waislamu, Waislamu walijitetea na wako kwa Constitution ya sasa na walijitetea wakasema, they have personal law to do with marriage, death, inheritance and succession na wakasema hiyo wanataka iwe hapa, okay haya wacha tuendelee. Tuendelee? Mzee umeelewa kile nilikuwa nakuambia? Mzee wa Kanisa, wazee wa Kanisa wako wangapi na akina mama? hebu nione mikono. Haujisikii vibaya Waislamu na Wahindu wako hapa lakini ...(Inaudible) haya, wacha tuendelee.

Haya, hapa tuko na sehemu sura ya pili, sikizeni hapa ndio tunazungumzia Jamhuri ya Kenya. Kama mnataka kuzungumza nyinyi watatu endeni hapo nje kidogo mkimaliza mtarudi. Ukitaka kuzungumza utakuja hapa mbele lakini iwe-relevant.

Speaker: ...(Inaudible)

Com. Adagala: Sijui kwa sababu nimetoka kwa sura moja naenda kwa ingine sasa sijui unataka... Let me tell you Banyore amkeni. Tumeenda mahali kwengi watu wako sharp na kitu najua Wanyore ni sharp lakini hapa mnajifanya. I am telling you, hii mambo ni mambo ambayo itakutawala mpaka kitandani mwako, mpaka kanisani, mpaka market na mmesema akina mama wako market watajuaje? Si mambo ya kucheka. Si mambo ya kucheza, si mambo ya kucheza.

Okuomi Francis: My names are Okuomi Francis, I am concerned with the laws of Kenya that is part 5, that section (d) where it talks of Islamic and Hindu personal law. I propose that we should also include Christian personal law because it is also a religion in Kenya, otherwise it is not complete.

Com. Adagala: We(Inaudible)

Okuomi Francis: We have got issues pertaining marriages in the Christian society so sometimes if it is not covered here it may bring problems in future.

Com. Adagala: Like what problems?

Okuomi Francis: Where a man is supposed to keep one wife but when we look at other religions like the Islamic Religion they have allowance for more women, so this one should be included so that we are well protected or women are well protected for that matter.

Com. Adagala: What denomination are you?

Okuomi Francis: I am a Christian.

Com. Adagala: What denomination are you, you don't even know what denomination is about?

Okuomi Francis: Church of God.

Com. Adagala: Ndio anauliza huyu mzee na umefanya mzaha hapa. Wazee wa Kanisa this is just a member speaking and saying something important and you are not picking it up theologically and it will never be down unless you said in a manner in which it fits in here. Inaonekana kama you don't mind, I think that is why when you take money to a Church wanakubali wanasema huyu ameleta sadaka mzuri wacha tufanye sadaka takatifu, alete marafiki zake halafu anaenda analeta rafiki zake anapeana pesa hakuna mtu kanisani anauliza hizi pesa zimetoka wapi. Hata kama huyu mtu ameuwa mtu na kutoa hizo pesa hawajali. Christian principles are not enshrined here because Christians themselves don't leave by them. Mtu anakuja tu Kanisa Jumapili anaenda, Waislamu wanaishi na sheria yao hata walitaka sharia law, North Eastern na Coast wanataka sharia

law kama ile ya Khartum hawataki hii mambo ingine, they want to leave by their religion only. Tulikuwa na very difficult time during civic education because they were just saying but we have a Constitution it is the Quran, lakini lazima tuishi na watu wengine tunawabembeleza halafu mwishowe wanasema yaa lakini sharia law iko. Hata wale watu wameenda huko juu watakuwa na shida, si sharia law peke yake, Chief Kadhi yako hapa. Haya, mzee si majadiliano. Sura ya pili, Jamhuri.

You can't be thinking now on your toes, it is something you should be living with.

Okuomi Francis: ... (Inaudible)

Com. Adagala: That's why it is not here.

Okuomi Francis: ... (Inaudible).

Com. Adagala: Mzee, Waislamu kuna tofauti tofauti lakini wote wanaenda na law of the... that is why mnapuuza mambo ya Kikristo ndio haiko hapa, hawa hawapuuza mambo yao.

Haya, the republic, Jamhuri: Kenya ni nchi ambayo inajisimamia hakuna mtu mwengine atakuja kusimama juu ya Kenya hiyo ndio kuwa sovereign republic. Mtu mwengine hawezi kutokea kule na aje kusimama ati yeye ndio mkuu wa Kenya, mtu wa nje au nchi ingine ije kusimamia hiyo itakuwa sasa ni vita kwa sababu Katiba itakuwa imevunjwa, sasa hiyo ni vita. Mnasikia kila mara kuna ugomvi kati ya Rais na Mabalizi, inasema Kenya is a sovereign republic. Kwa sababu wengine wanataka waje walete mambo ambayo itatawala Kenya kwa sababu wanatoa pesa kidogo kidogo hapa na pale, wanataka sasa Kenya iwe kama chini ya nchi zao na ni struggle, si kusema tu hapa lazima sovereignty must be guarded. There is a saying, najua Wanyore wanapenda Proverbs, there is a saying, 'the price of freedom is internal vigilance.' Mmewahi kusikia hiyo wengine? The price of sovereignty is internal vigilance, kwa sababu kuna highlands hapa Busia na Rarieda na Bondo na Wakenya wanauwawa hapo kwa sababu Uganda says these are their highlands, Kenyans go there and if they want to fish or even people live there and they tell them, this is Uganda so all those things now will have to be cleared.

Kuna triangle ingine hapo juu Turkana pia kuna dispute fulani, all those things will have to be settled, okay. Msingi yake ni vile tumesema demokrasia, utawala bora na pia Multi Party, hii multi party tumepigania muda mrefu hii pia itakuwepo, iko kwa Constitution sasa, haiwezi kutolewa, haiwezi kuwa tena mtu anakuja anasema baadaya isipokuwa wananchi waulizwe, mnataka turudi kwa one party rule, itakuwa referendum ndio ibadilishwe na iwezi tu watu wanakuwa mahali na wanasema iwe one au Parliament peke yake, okay?

Kuna nguvu za serikali zile ambao watu wamepeana kwa serikali na hizo zinafaa zikae kila moja itatengwa iwe ni nini. Itakuwa kati ya Bunge, Urais na pia Mahakama, zinafaa zikae, ni kama vidole hivi, zinapata nguvu huko lakini hapa lazima zikae tofauti

ndio zitaitwa Arms of Government.

Kuna haki za binadamu lazima ziheshimiwe kwa republic na pia sheria ndio itaongoza, huwezi kufanya kitu kiholela holela na ikubaliwe, lazima sheria isimamie kila kitu. Haya hapo ramani ya Kenya, eneo ya Kenya ni nini? Na hiyo yote iko kwa first schedule kueleza kinaganaga ya kwanza iko huku nyuma kwa Katiba yenu mtaangalia baadaye, inaeleza Kenya ni latitude, longitude, inapitia wapi, hapa bahari inasema, huko kwa ziwa Victoria inasema, hayo yote iko kwa first schedule.

Kwa Katiba ya sasa hakuna kitu kama capital ya Kenya, mnaweza kuketi hapa sasa nyinyi wenyewe mu-declare kama Katiba ijabadilishwa musema Lwanda ndio capital ya Kenya, mtu yoyote anaweza kusema mnaona. Hasa sasa Wanyore wanaweza kusema tu na hizo nguvu zoa za kawaida. Wasema Lwanda ndiye *yene*. Hakuna mtu atapinga, sasa inasemekana Nairobi ndio Capital ya Kenya.

Parliament, Bunge itazungumzia mambo ya Nairobi. Hiyo Capital tutazungumzia baadaye hapa mbeleni iko lakini pia kuna vitu vingine vitabadilika. Kitu kimoja wacha niwaambie sasa ndio mshike tukifika hapo mtaona. Capital ya nchi si sasa kila idara na kila Wizara iwe uko na kila ofisi kuu iwe huko. Huenda Parliament ikifanya itengeneze ati tutakuwa na kikao cha Bunge Nakuru au sasa tutaenda Isiolo, au sasa tutaenda tukae Busia au Kakamega hasa kwa Provincial Headquarters. Haitakuwa lazima Parliament iwe tu huko Nairobi na pia kuna sehemu ingine inakuja ambayo itasema idara na wizara na hizo vitu vyote vinafaa vitawanyike kwa nchi ili isiwe tu mahali pamoja Nairobi, okay? Hiyo ni part of devolution.

Lugha: Official lugha ya Kenya sasa ni Kiingereza sivyo? National language ni Kiswahili lakini sasa tumeweka lugha ya rasmi ya Kenya itakuwa Kiswahili na Kiingereza. Usisema Kiingereza na Kiswahili, zitakuwa in that order, Kiswahili na Kiingereza. Juu yake Kiswahili ni National language. Maana ya hii itakuwa kila kitu ambacho kimeandikwa haswa lugha yoyote hata ile ya hansard, huyu mama anatoka kwa hiyo Hansard ya Parliament lazima itakuwa kwa lugha mbili. Hapo kwa wakati huu kama Nasir Bin Taif akifanya submissions zake huko Parliament kwa Kiswahili kizuri sana wanaenda iko kwa tape kwa Kiswahili lakini ikiandikwa kwa record wana-translate. Mnaelewa? Mwisho hata Nasir siku hizi hapeani submissions kwa Kiswahili, mnajua hivyo. Watu wachache sana kwa Parliament wanazungumza kwa Kiswahili, mnajua hivyo? Wengi wao wameenda kwa Kiingereza kwa sababu Kiswahili hasiko rasmi kwa Katiba ya sasa lakini kwa hii hata sign kwa nyumba lazima siwe kwa hizo lugha mbili na juu yake hii lugha ya national language ni Kiswahili.

Haya, tunakuja kwa dini, serikali na dini zitakuwa tofauti. Nasema hivyo kwa sababu kuna nchi zingine uko kama Saudi Arabia, Vatican serikali na dini ni kitu kimoja na Iran. Inaitwa Islamic Republic hata Libya na hiyo ndio dini na wote wako chini ya hiyo. Sasa hapa hatutakuwa na hiyo na pia hatutakuwa na dini moja ambayo itakuwa dini ya serikali, State Religion hatutakuwa na hiyo. Na serikali itaheshimu kila dini lakini haitachukua dini moja iseme hii ndio dini ya serikali. Kama Vatican huko ni Roman Catholic na mkuu wa hiyo State anaitwa nani? Pope, hiyo ni head of State of the Vatican.

Kuna ile ishara ya taifa na hiyo iko kwa kinaganaga kwa first schedule, mtaona description yenyewe. Schedule ni kitu ambacho kinalete description ya hii sheria iko hapa. Kuna bendera yetu na iko hapo kama ishara, ukienda huko United National iko bendera mia moja na themanini na sita, ukiangalia tu unaona hii ni ya Tanzania, hii ni ya United States, hii ni ya Kenya, ikisimama inamaanisha Kenya na inafaa ijulikane ni nini ndio wamekeka kwa schedule hapo.

National Anthem; hiyo ni Wimbo wa Taifa na hiyo wanaita crown lakini tunaita crown kwa sababu it was from the crown, from the Queens or the Kings crown lakini kwa tafsiri ya kiswahili bado wanatafsiri hiyo nakala na kuna muhuri wa serikali. Hiyo pia itakuwa ishara ya Kenya.

Sorry, nimechoka kwa sababu jana nilifanya kazi nyingi sana. Kiapo iko kwa forth schedule, hiyo itakuwa hapo imekuwa described watu wengine kama wale quakers hawainui Bibilia kwa sababu kwa Bibilia inasema usiinue, swear tu “jes to jes, nay to nay” hiyo inaitwa affirmation. Tena tuna watu wengine ambao hawaamini Bibilia au Quran hao pia wanafanya affirmation.

National Holiday: Sasa kuna national holidays na hiyo ni Madaraka Day June 1 na Jamhuri Day, December 12 na siku ile ya Katiba Day, siku ile ambayo Katiba itatekelezwa. Hizo zitakuwa National Days. Hiyo ndio republic sasa. Kuna kitu ambacho mtu angependa kuongeza au proposal au kiti kitatuletea mwangaza?

Kaizer Amatalo: Naitwa Kaizer Matalo. Nataka kupendekeza hivi kuhusiana na State na Religion. Tumesema State na Religion vitakuwa tofauti lakini ni lazima State ichukue authority na iwe inafuatilia vile vitendo vya kila dini kwa sababu tukisema tu State na Religion ziko tofauti watu wataanza kufanya maneno yao huko pasipo kujali ati State inafanya nini. So State should come up with ways of monitoring the activities of this diverse religion that we shall have.

Com. Adagala: Kama unamwambia mmbwa achunge nyama. How would you want this done because the State will now dictate what should be preached. Come forward and you tell us how that affect freedom of expression and freedom of choice.

Kaizer Amatalo: We are aware that there are human rights and kuna dini fulani kama dini ambazo huja na zinasema ni dini halafu zinaanza kufanya vitendo kama tusema kutairi akina mama hivi na inasema ni dini. Sasa ikiwa serikali itasema tu, kila dini sasa ina uhuru wake vitu kama hivyo vitaweza kuharibu watu sana. Sasa ni juu ya State wenyewe kuhakikisha kwamba though tumepatia kila dini uhuru wake lakini vitendo vyo kila dini lazima viwe isipite mipaka fulani kuumiza haki za wanadamu.

Com. Adagala: Okay, kuna mtu mwingine. Dot com wako werevu sana. Kuna mtu mwingine alisema inafaa tuongeze hapo na wewe umesema pia. Dini isidhulumu mtu...tumeandika lakini hiyo nataka kukuambia kuna mtu mwingine kwa station ingine alisema hivyo pia. Dini isidhulumu mtu, yaani hizo human rights.

Fred Osome: Jina langu ni Fred Osome.

(Interjection)

Com. Adagala: Nataka ufikirie pia vipi dini inaweza kukaa, itakuja baadaye lakini nataka ufikirie hasa za Kikristo. How should they...it is not really monitoring in a way but even if they have to be monitored or to be supervised, how should this be done, what should be formed? You always have to have, umesema kitu but how should it be done? I want you to think about that.

Fred Osome: Jina ni Fred Osome. Chapter 2, Republic section ya territory, section seven part (ii). The republic is divided into districts and provinces set out in the second schedule. Hapa kuna swala nyeti, swala la mipaka kwa sababu hapa nyuma ...

Com. Adagala: Toa pendekezo.

Fred Osome: Pendekeza langu ni kwamba hivi districts and provinces zenye zimekua set out in the second schedule zitupiliwe mbali, wananchi waulizwe kwanza mipaka ya districts na provinces zitakuwa wapi kabla hazijawekwa hapa. Kwa vile inaonekana kwamba hii Constitution mpya inataka kupatia districts ambazo zilikuwa created na mtu akitangatanga tu ovyo ovyo...

Com. Adagala: (Inaudible)

Fred Osome: Inaonekana kwamba hii Katiba wants to give the force of law, section of the districts and provinces which were created by somebody for political gain. So I am proposing that all the districts and the provinces set out in that sections be repealed and new boundaries created so that we don't have problems with Trans Nzoia and Western Kenya and Maseno where by sections of Maseno, infact somebody formed the boundary where some section is in Vihiga and all districts and provinces in this country. It will not be proper to give a false law to this system if we are creating these without consultation of the Kenyan people.

Com. Adagala: I hope you know it includes Vihiga District. We can say also even the first 42 were not by consultation sababu mikono ndio alipiga tu ruller but kijana unajua mtu akirudi pale hasikii tena. We have a boundaries Commission, eleweni hatukutaka kutingiza kila kitu Kenya, tukianza hivyo mtakuwa kwa hii jambo nyumba ya mtu imekatwa hivi. Kweli it is a violation of human rights lakini kuna mambo mengine makubwa ya Constituion ndio tulitaka tuangalie sasa. Sasa tulisema tutahifadhi hizi boundaries including provincial ones and believe me North Eastern kwa sababu nilikuwa huko nikifanya hearings and civic education wao watakuja na moto kwa sababu kuna provincial headquarters yao na it is in Coast Province. Wewe wacha hii mambo, the Provincial Headquarters for North Eastern is in Coast Province mnaelewa? Mipaka wamekata hivi na hiyo is in Tana River. So we have put a boundary Commission kwa sababu ni kitu kinafaa, hatuwezi kumaliza hiyo wakati huu

kweli?

Sasa boundaries Commission itakalia hayo yote, tutazungumza mambo ya Commissions mbele lakini umesema vizuri only that even the other 42 districts, no one was consulted they were made by the colonial Government. So you were right, that submission you should keep it, the boundaries Commission will come, you should develop it, you are a young man. Develop it even look at the map don't just give hii peke yake kuna zingine huko Hamisi, Wakalenjin pia wanasikia wawe kule au nini. Zingine Lugari imesongeshwea mara tatu au mara nne hivi ikuchukua sehemu ya Western inaenda Rift Valley. Kuna zingine kama hiyo ya Garissa, so sit down and make a good submission about that and wait for the boundaries Commission, okay.

Speaker: Mimi nataka....

(Interjection)

Com. Adagala: That is why we have come to you. Professor Ghai alisema the Commission does not have all the wisdom, it does not have a monopoly of the wisdom that is why we have come back to you. So be very alert and if I make a suggestion to you like develop your argument young man, you do it because it should be something that will be about 10 pages long if you do it.

Mr. Lukose: Mwenyekiti kuhusu State and Religion nakubaliana kabisa na number 2. There shall be no...

(Interjection)

Com. Adagala: ...(Inaudible)

Mr. Lukose: Jina langu naitwa Lukose.

Com. Adagala: Utasema jina kila mara.

Mr. Lukose: Every time I come I must say that, okay.

Com. Adagala: So that this information does not get lost so that your grand children will not miss.

Mr. Lukose: Hii ni kweli kabisa kwamba kuwe na tofauti katika serikali ama nchi na dini lakini kitu nimetaka Constitution itasema kitu gani kuhusu kitu kama Kenya Broadcasting Corporation inavyotumiwa na religion sawa sawa ni kitu ambayo ina-promote religion. TV inatumika kutangaza mambo ya dani kuliko kutangaza mambo ya maendeleo na hii KBC ni mali ya wananchi wa Kenya.

Com. Adagala: Okay KBC ni mali ya wananchi wa Kenya na pia ni Biashara. Hawa watu wanaenda ... (Vernacular). Hiyo KBC watu wanaenda hapo kama huyu Wairimu analipa lakini kuna sehemu fulani lazima wafanye mambo ya maendeleo. Hata hivyo kuna sehemu hapa ya information in the bill of rights. A whole section on the press and all that lakini it is an interesting point put it down for mzee. We take all your proposals, even if I comment on them we write it down.

Scholastica Naliaka: Kwa majina naitwa Scholastica Naliaka Ndale. Mimi ninaonelea pendekezo langu, chapter number 3 inaonekana ya kwamba.

Com. Adagala: We have not reached chapter three.

